# Learning by Ear – Religious Dialogue: "A Bridge over Gori"

## Episode 01: "Kwenye Chuo Cha Ubuntu!''

**Author: Romie Singh**

**Editors: Katrin Ogunsade, Naïma Guira**

**Proof reading: Natalie Glanville-Wallis**

**Expert on African religions: Jean-Félix Belinga Belinga**

**KISUAHELI ERIC PONDA**

**List of characters for episode 1:**

- **Narrator /Philip, male (17)**
- **Harry, male (17)**
- **Mat, male (16)**
- **Layla, female (16)**
- **Roshi, female (16)**
- **Ishmail Omer, Layla's father (43)**
- **Hassan, Layla's brother (12)**
- **+ Students (background noise outside/singing in hall)**
- **+ Girls in the background (at Café)**

1. **SIG TUNE UP**

2. **INTRO:**

**Hujambo na karibu kwa Mfululizo wa vipindi vya NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO vinavyotayarishwa na Deutsche Welle. Katika mfululizo huu wa vipindi 10 katika tamthilia "DARAJA LA MTO GORI",, tunasikia hadithi ya kusikitisha jinsi SIASA na DINI zinavyo tumiwa kuigawanya jamii na kusababisha uhasama baina ya Jamii, na Familia Mbili na kadhalika penzi la Vijana wawili wanaolazimika kulificha kutokana na uhasama huo. Ungana Nasi uusikie umuhimu wa Majadiliano, Ushirikiano na uvumilivu wanapojaribu kuushuluhisha mzozo uliokita mizizi. Kwenye Makala hii ya Kwanza tunakutana na Harry, Layla na Marafiki zao. Wote hawa ni wanafunzi wa mwaka wa pili katika Shule ya Ubuntu ambao wanarudi shuleni baada ya likizo ndefu. Harry anaishi na mjombake ambaye ni Kasisi wa kanisa Katoliki, lakini maisha kidogo hayamwendei vizuri. Layla naye anashangazwa na tabia ya mdogo wake wa kiume.Maisha ya Familia yao yalibadilika ghafla miezi michache iliyopita,na kwa sasa lazima achangie katika ulezi wa mdogo wake. Philip ni miongoni mwa marafiki wa dhati wa Harry na ndiye atakaekusimulia kisa chote. Katika makala hii ya kwanza anaturegesha yalikoanzia, kwenye Chuo Cha Ubuntu!**

**Scene 1**

**Harry, Philip, Mat, students in background**

3. **PHILIP/NARRATOR:** **Gori ni mji wenye soko kubwa maarufu uliogawanywa na Mto.Hapa tunapanda Mahindi na Matunda. Miaka mingi tu iliyopita, Kilimo cha sehemu hii kiliwavutia wageni wengi kutoka pembe zote za Africa. Na ndio sababu kuna mchanganyiko wa watu wa asili tofauti , Tamaduni, rangi,lugha na Dini mbali mbali katika mji huu. Miaka kumi iliyopita kiongozi mmoja aliye elimika, Chifu Solomon Banda alikuwa na nadharia ya kuwa na jamii iliyoungana ya waAfrika kwa manufaa yao, kwahiyo akaanzisha Chuo cha UBUNTU,cha mafunzo kwa Vijana na wasichana wa umri kati ya Miaka 16 hadi 18, wa madhehebu mbali mbali .Nilijiunga na chuo hicho miaka miwili iliyopita.Kumbukumbu ya enzi hizo ni kama matukio ya jana! Tulifurahi kuonana tena baada ya likizo ndefu!**

4. **SFX Early morning. Learners assemble in school grounds, student's noise, birds**

5. **HARRY:** **Hujambo Philip?**

6. **PHILIP:** **Sijambo , unaendeleaje Harry.?**

7. **HARRY:** **Naendelea vizuri..!... lakini kama unavyojua si rahisi kuishi na Mjomba ambaye ni kasisi wa kanisa Katoliki!**

**8. PHILIP:** **Pole sana Harry,.. nakuonea huruma...! Vipi kuhusu ripoti yako shuleni?**

**9. HARRY:** **Si kama yako… najua wewe umepita kwa alama "A" katika masomo yote.**

**10. PHILIP:** **Ni kweli Harry, na safari hii Babangu alifurahi sana, ingawa Mama… hata hakutaka kushughulika nayo…..! Na wewe je?**

11. **HARRY:** **Mimi nilipata Gredi ya Kwanza katika masomo manne, na Gredi ya Pili katika masomo matatu. Wazazi wangu ,jamaa na marafiki nyumbani walifurahi kusikia habari hizo, lakini Mjombangu, huwa haridhishwi na chochote! Kila wakati analalamika tu…! *(CHANGES VOICE TO SOUND OLDER)* Kila wakati ni ..oooh.. Harry…., yule Philip atakupokonya nafasi ya kiranja wa shule iwapo hutakuwa mwangalifu!**!

12. **PHILIP:** **Mimi ? Haaah!... hata sifai kabisa kuwa mwanafunzi mkuu!**

**13. HARRY:** ***(Laughing)* Wewe? Wasichana wote wanapapatika, kweli umewazuzua , na mawazo yao yote ni kwako tu, na ndio sababu mimi hupenda kutembea na wewe wakati wote!.**

**14. PHILIP:** ***(Laughs)*** Aah wapi**….wacha mzaha..!**

15. **HARRY:** **Tutaendelea kufanya mambo yetu kwa pamoja! Na wewe utanifunza mambo ya mjini na ya wasichana warembo wa kisasa...! Sawa?**

**16. PHILIP:** *(laughing)* **Sam hubadiliki wewe!** ***Gonga tano basi …!***

17. **SFX: Smack palms of hands and click flingers**

**18. MAT:** ***(Off mic)*** **Philip, kiranja wangu!... Harry!! (deep voice)Twende kuleee.. uwanjani! Twende tukapigane miereka!**

19. **PHILIP:** ***(laughing)*** **Mat! – Rafiki yangu…! wewe ni mwandani wangu mkubwa!**

*20.* **MAT:** **Eti nini?... Sasa… mimi ni nani wako?, Rafiki au Mwandani? Chagua moja tu***!* ***(They all laugh)***

**21. SFX: BELL RINGS**

22. **PHILIP:** **Hah! Ishara ya kwenda darasani hiyo. Ni vizuri kurudi shuleni baada ya likizo ndefu!.**

**23. HARRY: Sasa, sisi ndio wafalme hapa, au ukipenda madume watatu Shuleni Ubuntu... Au vipi?**

**24. PHILIP+ MAT: Ndio.. ! Maisha marefu kwa madume wa Ubuntu!**

**AMBIENCE FADE OUT/CHANGE OF VOICE**

**25. PHILIP/NARRATOR: Na Kwa hakika tulikuwa madume: katika mchezo wa Kandanda, Mimi, Mat, na Harry tuliwika..!,- Madume wa Ubuntu!.**

**Kwa upande mwengine kulikuwa na Msichana Layla, Mrembo mwenye macho ya gololi na kiuno cha mviringo, ambaye kwa muda mrefu nimekuwa nikimtazama kila nikiwa darasani.Namtazama akitangamana au kusalimiana na wenzake.**

**<u>Scene 2. Outside /same college garden</u> Layla, Roshi, students in background**

**26. <u>SFX: student's noise, birds</u>**

**27. LAYLA: Roshi! Unaonekana mchangamfu sana , Je ulilfurahia likizo yako?**

**28. ROSHI: Ndio..! tulizuru maandari mbali mbali ya kupendeza na pia kuwa pamoja na Familia yangu. Ama kwa kweli nilikuwa na wakati mzuri sana,**

**29. LAYLA: Oohhh! Je kuna wavulana wengine wa kupendeza katika familia yenu?**

**30. ROSHI: Layla! Wapi jamani.. ! wavulana wote wa rika langu, bado wanaonekena wadogo sana..! Je wewe?**

31. **LAYLA: Mimi Kakangu huniudhi kila wakati, na Babangu naye hanipi nafasi ya kutoka nje ila tu kusoma na kusaidia kazi za nyumbani! Aliniamuru nikae ndani kila wakati ili nisichomwe na jua ili niendelee kuwa mweupe!**

32. **ROSHI: Ai..! Huo ni ukoloni mambo leo. Kwani hajasikia kwamba "weusi ni Urembo! *(laughs)* Na je kuhusu mazoezi yako ya kukimbia. Natumai bado unaendelea nayo.**

**33. LAYLA: Niliendeelea na mazoezi yangu kama kawaida …lakini chumbani mwangu nikiwa nimejifunika kutoka utosini hadi wayoni. Joto lilikuwa limezidi nje..**

**34. ROSHI: Layla! Itabidi tuwaulize wasichana wengine wa Kiislamu, wanavyofanya mazoezi.Wewe si msichana wa kwanza..!. Tunataka ufanye mazoezi zaidi ili uweze kushinda nishani nyingi zaidi za dhahabu kwa timu yetu!**

35. **LAYLA:** ***(laughs)*** **Hah! Kwa hiyo la muhimu ni mchango wa nguvu zangu… eeh ? Sivyo?**

**36. ROSHI:** Shule hii ya **Ubuntu ni shule ya wavulana na wasichana. Hivyo wanapaswa kushirikiana kwa kila jambo, liwe ni upande wa masomo au hata michezo!.Jaribu kumueleza Babako kwamba michezo ni sehemu ya utaratibu wa mafunzo Shuleni. Najua Mamako angependa kusikia haya.**

37. **LAYLA:** ***(sadly)*** **Ni kweli. Lakini kwa bahati mbaya hayuko karibu nami amshinikize Kakangu Hassan aje nyumbani siku moja!. Angeukomesha kabisa upuzi huu.**

**38. BELL RINGS**

39. **ROSHI: Kingele hiyo imelia..!. Sasa ni wakati wa mkutano wa asubuhi shuleni.**

**<u>Scene 3. In the Big Hall</u>**

**Philip, students singing**

**40. <u>Song: Ubuntu Anthem (song see extra document)</u>**

41. **PHILIP/NARRATOR:** ***(SPEAKING OVER ANTHEM)*** **Na kama ulivyotiririka wimbo wetu wa shule, ndivyo yalivyotiririka maji ya Mto unaougawanya Mji huu. Maji hayo yenye tope yanaugawanya mji huo kwa sehemu mbili na kuzitenganisha Familia mbili zenye ushawishi mkubwa katika jamii: Familia ya Harry, ya Mzee Dembele na Familia ya Layla ya Mzee Omer.Babake Harry, Chifu Bandile Dembele alikuwa kiongozi wa kitamaduni aliyeheshimika sana. Kijiji hicho hakikuwa na shule nzuri na hivyo Chifu Bandile akamuomba Kakake Barnabus ambaye ni Kasisi wa kinisa katoloki, kumpa nafasi Harry ya kusoma katika shule hii ya Ubuntu.Harry alimpa jina la utani la Askofu Baba Mdogo.Kwasababu ya urafiki wetu na Mat, Harry alianza kuzitambua anasa za mjini na akagundua kwamba kuna mengi zaidi ya kujifunza zaidi ya kuwa mwanafunzi bora na mfuasi mzuri wa kiKatoliki….!Laiti Mat angempa fursa!**

**Scene 4. In a cafe with music and pool tables**

**Harry, Mat, Philip, girls in background**

***42. SFX: Disco music/pool tables***

**43. MAT: Sasa twendeni …. Twendeni jamaani !**

44. **HARRY**: ***(protesting)*** **Hapana, Mat- Mimi na Suzie bado tunaendelea kujifurahisha hapa. Tusubirini kwa muda wa dakika 30 hivi!**,

**45. PHILIP:** ***(laughing)*****Pia mimi na Rachel tunahitaji muda zaidi!**

***46. Girl giggles***

**47. MAT:** ***(joking)*** **Hata hamna haya nyinyi wawili. Kasisi mtarajiwa..!. Na wewe Philip, Mtoto wa mhariri mkuu wa gazeti mashuhuri mjini. Sasa wazazi wenu watasema nini wakiwakuta hapa?**

***48. SFX: Pool playing***

49. **HARRY: Sisi tunacheza tu mchezo wa** *Pool.* **Hata hivyo nawanajutia ambao hawakuandamana nasi maana wamekosa mengi**!***(laughing)***

*50.* **MAT:** ***(more serious)*** **Sikilizeni hapa mimi ndie mwenye gari, na kama hamutaki kwenda sasa, msinilaumu kwani mtalazimika kutembea!**

*51.* ***<u>Philip + Harry complaining and saying goodbye to the girls.</u>***

**<u>CUT AMBIENCE/CHANGE OF VOICE</u>**

52. **PHILIP/NARRATOR: Wakati huo huo,upande wa pili wa Mto, Familia ya Omer wanakula chakula cha jioni. Babake Layla alifiliwa na Mkewe baada ya kuugua saratani miaka michache iliyopita, na sasa ameachiwa jukumu la kuwalea bintiye Layla na Mwanawe wa kiume Hassan. Ni mfanyabiashara aliyestawi na pia mwanachama wa baraza la mji wa Gori. Anaulalamikia ushawishi wa Kasisi Barnabus anayezidi kuwa maarufu katika eneo hilo la Gori. Malengo yao ya kibiashara yameanza kugongana kwasababu ya mitazamo tofauti naye Hassan ameanza kujifunza itikadi kali kutoka kwa wavulana wakubwa katika chuo cha Madrassa anachohudhuria. Jambo linamtatiza sana Layla**.

**<u>Scene 5. At home</u>**

**Mr. Omer, Layla, Hassan**

***53. <u>SFX: Supper/utensils, dishes</u>***

54. **MR OMER:** ***(talking while munching)*** **Unajua Layla Kasisi Barnabus anazidi kuwa na ushawishi mkubwa katika eneo hili. Anakitaka kipande kile cha ardhi kinachotaka kutumiwa na Baraza la Waislamu. Lakini sisi ndio tuliokuwa wa kwanza kuwasilisha maombi.**

**55. LAYLA: Anataka kukifanyia nini?**

**56. HASSAN: Kwani Mkristo anahitaji sababu kwa Muislamu? Ni kwamba anaupiga vita Uislamu tu.**

57. **LAYLA: Hassan, hatuhitaji mazungumzo ya aina hiyo kwa sasa. Kwanza unajua nini kuhusu Ukristo na Uislamu?. Wewe una miaka 12 tu…!**

**58. HASSAN: Wewe unasoma kwenye chuo kisicho na maana cha Ubuntu ambako wanasema hakuna dini moja iliyo na majibu yote ya kitendawili cha maisha.Lakini nakuhakikishia kwamba iko! Mimi nasoma kwenye Madrassa na najua iko**!.

**59. LAYLA: Basi unapaswa kuelewa kwamba kwamba Wakristo na Waislamu wanamuabudu Mungu mmoja tu. Sisi Waislamu tunaamini Yesu ni mmoja wa watume na Mamake Mary ni mwanamke muhimu anayempenda Mwenyezi mungu.**

***60.* HASSAN: Hakuna mungu mwengine isipokuwa Allah *(shouts)* Mungu ni mkubwa!**

***61. SFX: CELL PHONE RINGS***

62. **MR. OMER: Shhhh! nyamaza Hassan tafadhali!**

***63. SFX: PICKS UP CELL. RING STOPS***

**64. MR. OMER:Ishmail Omer hapa….ndio…ndio, Alhamisi tarehe 11, Sawa, ndio .. (*FADE)* Nazihitaji takwimu za mkutano wa mwisho.. hh pia umfahamishe Bw Lay Layton Browne. Yule mhariri mkuu wa gazeti hapa mjini. Tunataka Gazeti la Gori Tribune lichapishe habari hizi.**

**AMBIENCE FADE OUT/CHANGE OF VOICE**

**65. PHILIP/NARRATOR: Omer amekuwa akishughulikia biashara zake na kamwe hakuuona msimamo wa Hassan uliozidi kuwa mkali.Layla amekuwa akiyaona haya na anahisi ni mwanzo mbaya.**

**66. SIG TUNE UP**

**67. OUTRO:**

**Na hadi hapo ndipo tunapofika mwisho wa makala ya mwanzo ya Noa Bongo Jenga Maisha yako.Harry, Layla, Philip na marafiki zao wameanza mwaka mpya shuleni.Wote wamesisimka na kufurahia kurudi shuleni baada ya likizo ndefu, lakini hawakijui kinachowasubiri. Ungana nasi kwa sehemu ya Pili ya mchezo huu, ufahamu jinsi Philip atakavyoweza kupambana na changamoto yake ya kwanza. Na kumbuka ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki au vipindi vingine vya Deutsche Welle, tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de Hadi wakati mwengine Kwaheri kwa sasa.**